# Tathmini

## katika kiwango cha msingi na

## katika kiwango cha chini cha shule ya upili katika masomo ya lazima.

Bildungs- und Kulturdirektion des Kantons Bern

**(Seite 2)**



**Ujumbe kwa wazazi na walezi halali kuhusu tathmini katika kiwango cha msingi na katika kiwango cha chini cha shule ya upili katika masoma ya lazima.**

Ujumbe kuhusu shule ya chekechea, Basisstufe na cycle wa élémentaire uko katika tovuti ya wizara ya elimu ya kantoni ya Bern: www.erz.be.ch

**Jedwali la yaliyomo:**

Tathmini inayolenga uwezo……………………………………………………………………………………….4

Tathmini ya wanafunzi ni ………………………………………………………………………………………….4

Mathumuni kadhaa ya tathmini……………………………………………………………………………….5

Maamuzi kuhusu njia za elimu……………………………………………………………………………………6

Utaratibu wa kusonga kutoka kiwango cha shule ya msingi hadi kiwango cha shule ya upili cha chini………………………………………………………………………………………………………………………….7

**Kiambatisho**

-Kiambatisho 1: Madarasa yana maana hii.

-Kiambatisho 2: Njia ya tathmini katika kila kiwango

**Impressum**

**Published by**
Erziehungsdirektion des Kantons **Bern**

**Contact/Information**
Erziehungsdirektion des Kantons Bern
Sulgeneckstrasse 70, 3005 Bern
031 633 85 11

akvb@erz.be.ch
2. Auflage Februar 2018
#826381v1

**(Seite 3)**

**Tathmini katika kiwango cha msingi na kiwango cha chini cha upili 3**

……………………………………………………………………………………………………………………………………

Wazazi wapendwa,

Kitabu hiki kinawapatia ujumbe kuhusu kutathminiwa kwa wanao na maamuzi yanayohusu njia ya masomo ya watoto wenu. Ukihitaji ujumbe zaidi, tafadhali tazama tovuti yetu www.erz.be.ch au zungumza na walimu wa darasa ama mwalimu mkuu wa shule.

Tafsiri za kitabu hiki ziko katika lugha tofauti na pia katika tovuti ya wizara ya elimu ya kantoni ya Bern www.erz.be.ch.

Wizara ya elimu.

**(Seite 4 )**



## Tathmini inayolenga umahiri

Sababu kuu ya tathmini ni kuchochea kusoma na kukua; nia ni mtoto wako kuhisi tathmini ni ya kusaidia masomo yake. Umahiri wa Lehrplan 21 unatoa alama za muelekezo kwa walimu wanapo watazama na kutathmini wanafunzi.

## Tathmini ya wanafunzi ni…

**…. Inalenga kukuza masomo na kukua kiakili.**

Utathmini na kupeana majibu kunachochea kusoma na kukua kwa watoto na waliobalehe kwa kutoa mwongozo wa jinsi ya kukaribia hatua ifwatayo ya masomo.

**…. inaambatana na somo**

Kutumia matukio katika somo ndio mojawapo ya sehemu ya kila tathmini.

**…Uwazi**

Tathmini inawapatia wazazi ujumbe wa kueleweka na uliotofautishwa kuhusu maendeleo na kukua kimasomo kwa mwanao wa kike au kiume.

**…wenye kina**

Tathmini inaangazia yote, umahiri wa maelezo maalum, na baina ya mitaala.

Umahiri wa maelezo maalum unapatikana kutoka kwa masomo tofauti kama (kijerumani, hisabati, muziki n.k) umahiri baina ya mitaala, ni kama vile kujitegemea au kufanya kazi kwenye

kundi ,fanya jukumu la maana katika masomo yote.Umahiri wa maelezo maalum na wa baina ya mitaala yameshikanishwa pamoja katika muktadha wa maelezo.

**(Seite 5 )**



……………………………………………………………………………………………………………………………………………

## Mathumuni kadhaa ya tathmini ya wanafunzi.

**Tathmini na kusaidia mchakato wa kusoma**.

Sababu kuu ya masharti ni kusaidia mchakato wa kusoma kwa mwanao kikamilifu. Hii ndio sababu walimu huwatazama wanafunzi mara kwa mara kwa msingi wa vigezo viliyochaguliwa. Walimu wanatumia kile wanachotambua kutoka kwa mitazamo hii kupanga masomo yao ifaavyo, Vile vile kutoa mapendekezo mwafaka katika mikutano baina ya wazazi na walimu.

**Tathmini kwa maendeleo ya kimasomo.**

Baada ya kukamilisha kwa sehemu kubwa za masharti, walimu wanatathmini ni kiwango kipi wanafunzi wametimiza malengo yanayo husika na masomo hayo, kwa kutumia bidhaa mitihani na mchakato wa kusoma kufanya hivyo.

Wanafunzi wanafahamishwa kuhusu malengo na vigezo pale mwanzo wa mpangilio wa somo.

**Tathmini ya kibinafsi**

Wanafunzi wanatumia utathmini wa kibinafsi ili kupima umahiri wao wa maelezo maalum, na baina ya mitaala katika muda wa mwaka wa shule. Kwa kufanya hivo wanaangazia kusoma kwao

na wanachukua jukumu la mchakato wao wa kimasomo. Tathmini ya kibinafsi hufanywa katika kila somo ndani ya muktadha wa hali ya kimasomo.

**Mkutano baina ya wazazi na walimu.**

Mkutano baina ya wazazi na walimu unaofanyika mara moja kwa mwaka, huwezesha kukuuza uamainifu na ushirikiano baina ya wazazi na walimu. Huchangia mawasiliano baina ya wazazi na walimu na kuwezesha kutofautisha matokeo ya tathmini ya kibinafsi ya wanafunzi na ule wa walimu na wa wazazi wao. Mikutano ya wazazi na walimu huwezesha kuwa zawadia kwa matokeo mazuri  na tabia njema kupewa heko kwa njia ifaayo.Vile vile,huwezesha wazazi na walimu kutazama matatizo ana kwa ana na kuafikia  makubaliano ya pamoja jiinsi ya kuendelea mbele.Shule itapanga mikutano zaidi ya wazazi na walimu inayohusiana na matukio maalum au kwa ombi la wazazi.

**Rekodi ya mkutano wa wazazi na walimu**

Maswala yatakayo jadiliwa yatatiwa sahihi; maelezo mafupi yanaweza ongezewa iwapo itahitajika. Makubaliano ya ujumla na wazazi yanaweza yakanakiliwa chini kwa ufupi katika sehemu iliyotolewa kwa ajili ya hayo. Iwapo makubailiano ya ujumla hayatahitajika, sehemu hii itabaki bila maandishi. Fomu hii ni baadhi ya folda.

**Kwingineko ya umahiri wa kibinafsi na umahiri muhimu**.

Umahiri wa kibinafsi na umahiri muhimu ni baadhi ya umahiri baina ya mitaala tofauti. Tathmini ya umahiri huu itarekodiwa katika fomu tofauti baada ya miaka 7, 8 na 9. Wote walimu na wanafunzi wanatathmini umahiri huu.

**Ropoti ya tathmini**

Ripoti ya tathmini inawapatia wanafunzi matokeo katika maandishi ya kiwango chao cha mafanikio katika masomo tofauti.

Wanafunzi hupokea ripoti ya tathmini.

***Kiwango cha msing:****;*

-Katika mwisho wa miaka,2,4 ,5 na 6

***Kiwango cha chini cha upili:***

-Katika mwisho wa miaka 7,8 na 9

Ripoti hizi za tathmini zinatokana na uamuzi wa kitaalamu wa busara, wa walimu na wala sio kwa kuhesabu wastani.

**(Seite 6 )**



## Maamuzi kuhusu njia za elimu

Maamuzi kuhusu njia za elimu hufanywa kwa kuzingatia utathmini wa kina. Kati kati ya mchakato wa kufanya maamuzi kuna swali la darasa lipi, aina ipi ya shule, au kiwango kipi cha mahitaji kitakuwa mwafaka zaidi kwa kusoma na kukua.

Hasa katika maamuzi kuhusu njia za elimu vinavyohusika ni:

-Kuingia katika mwaka ufwatao wa shule;

-Kuruka au kurejelea mwaka katika shule;

-Kupelekwa katika darasa maalum au kuacha darasa maalum na kurudi katika darasa la kawaida;

-Kupelekwa au kuanzia au kubadilisha hadi katika aina maalum ya shule au kiwango cha mahitaji maalum katika kiwango cha chini cha somo la shule ya upili;

-kuingizwa katika programu ya baccalaureate la kiakademia, kiwango cha shule ya upili cha juu cha kibiashara, shule ya upili ya kiwango cha juu ya taaluma maalum au shule ya baccalaureate la ufundi.

**Maamuzi ya kibinafsi kuhusu njia za elimu.**

Maamuzi ya kuhusu njia za kibinafsi za kielimu yanaweza fanyika wakati wowote katika muda wa masomo ya kilazima, ikiwepo katikati ya mwaka wa kanuni. Maamuzi kama hayo hufanywa kwa msingi wa kesi moja kwa nyingine kwa kila mwanfunzi binafsi inavyohitajika na kupewa wasia. Mfano, mwanafunzi binafsi anaweza akabadilisha darasa katikati ya mwaka na kuenda darasa maalum au kuenda kiwango chenye mahitaji ya chini au ya juu katika kiwango cha juu cha shule ya upili.

Maamuzi kuhusu njia za kielimu huchukuliwa na mwalimu mkuu kupitia ombi la mwalimu wa darasa. Hao huwasiliana na wazazi kwa kuandika ripoti ya tathmini au katika taarifa ya uamuzi wa njia ya kielimu ya mtu binafsi.

**(Seite 7 )**



# Utaratibu wa kusonga kutoka kiwango cha shule ya msingi hadi kiwango cha shule ya upili cha chini

## Kiwango cha shule ya msingi na cha shule ya upili cha chini.

-Neno **’Kiwango cha msing**i’ humaanisha miaka ya 1 hadi ya 6.

-Nen**o’kiwango cha upili cha chini**’ humaanisha miaka ya 7 hadi ya 9, bila kuzingatia njia ya kimasoma inayofuatwa au aina ya shule au mahitaji ya kiwango(Niveau) kinachohudhuriwa. Katika kiwango cha shule ya upili cha chini, wanafunzi huwa wanahudhuria kulingana na mojawapo ya mahitaji matatu ya vitengo: *Realschule,sekondarschule,au kitengo cha* mahitaji ya *special secondarshule*(iwapo mkoa unapeana kiwango hiki).Mahitaji katika kiwango cha

*sekundarschule* ni mengi kushida yale mahitaji ya kiwango cha *Realschule.* Kuhama kutoka kitengo cha shule ya upili cha chini huchukua muda wa miaka 6.

**Mchakato wa kuhama**

Lengo la mchakato huu ni kuhakisha kwamba mwanao anapelekwa kwa aina ya shule na kiwango cha mahitaji ya mada maalum ambacho ndio bora zaida kwa kusoma kwake na kukua. Kuwezesha maendeleo ya mwanao hutazamwa katika muda mrefu, kutazamwa huanza mapema katika mwaka wa 5. Tathmini ya sababu inayowezesha maendeleo huzingatia yafawatayo:

-Tathmini ya umahiri katika masomo maalum kwa masomo kama vile, Kijerumani, Kifaransa na hisabati; Tathmini ya mwaka wa 5 na ripoti ya uhamisho ni mojawapo ya chanzo msingi cha kupewa darasa lifwatalo.

-Tathmini ya kibinafi ya umahiri katika kila somo;

-Maoni ya wazazi;

-Tathmni ya kibinafsi ya mwanafunzi.

**Ripoti ya uhamisho**

Mwalimu wa darasa hutayarisha ripoti ya kuhama kwa kuzingatia majadiliano na walimu wengine wanaofanya kazi pamoja darasani. Ripoti hii inatoa habari kuhusu umahiri wake katika masomo ya, Kijerumani, Kifaransa na Hisabati na vile vile tathmini ya kibinafsi katika masomo yote katika muhula wa kwanza wa mwaka wa 6.

**Faili ya uhamisho**

Faili ya uhamisho iko na maandishi matatu tafauti:

-Uteuzi kwa mtazamo wa walimu;

-Tathmini ya kibinafsi ya mwanafunzi;

-Uteuzi kutokana na maoni ya wazazi.

Faili ya ya kuhamishwa unatumika kama msingi wa mkutano wa uhamisho.

**Mkutano wa uhamisho**

Ndani ya au kabla ya mwisho wa mwezi wa Januari katika mwaka wa 6, wazazi hupokea ripoti ya uhamisho na faili ya uhamisho zikiambatana na ombi la maoni yao. Baadaye, wazazi na wanafunzi hualikwa katika mkutano wa uhamisho na mwalimu wa darasa. Nia ya mkutano wa uhamisho ni kuunda ombi la pamoja la uteuzi. Baada ya mkutano,mwalimu wa darasa huongeza ombi, hili likimlenga mwalimu mkuu wa shule, katika faili ya uhamisho.

**Mtihani wa tathmini tena**

Iwapo wazazi wa mwanafunzi  na walimu hawataweza kuafikiana kwa ombi la pamoja uteuzi maalum, wazazi watamsajili mwanao kwa mtihani wa tathmini tena wa kantoni kwa nji aya faili ya uhamisho. Mwanafunzi lazima afanye mtihani wa masomo yote husika kwa uteuzi (Hisabati, Kijerumani, Kifaransa) hata ingawaje wazazi na walimu wanaweza kuwa  wanatofautiana kwa somo moja au mawili. Mwalimu mkuu wa shule ya msingi kwa hivyo atafanya uamuzi wa uhamisho kwa kuzingatia matokeo ya mtihani wa tathmini. Masharti tofauti hutumika kwa wanafunzi wageni ambao wana asili ya lugha tofauti ,wale ambao wameingi majuzi katika Kantoni na wale ambao hawawezi hudhuria shule kwa sababu za kiafya na wale wenye upungufu wa kusoma.Walimu na wazazi watapata mahitaji ya mtihani na ujumbe zaidi kuhusu mtihani wa tathmini tena katika tovuti ya wizara ya elimu. (www.erz.be.ch)

**(Seite 8 )**



**Umuzi wa uhamisho**

Uamuzi wa uhamisho utafanywa na mwalimu mkuu wa shule ya msingi kwa kutumia faili ya uhamisho. Wanafunzi ambao watapelekwa katika kiwango cha *sekundarschule* au kiwango maalum cha *sekundarshule* (iwapo mkoa unapeana kiwango hiki) angalau masomo mawili baina ya matatu husika katika uteuzi huchukuliwa kuwa wanafunzi wa shule hiyo.

Masharti maalum huongoza uhamisho katika shule ya upili ya chini katika kantoni yote ya Bern. Mwalimu mkuu wa shule ya msingi anaweza akasusia masharta hayo ya tathmini na mchakato wa uhamisho iwapo wanafunzi wametoka katika asili ya lugha tofauti ambayo wamehamia kantoni hivi karibuni na wale watoto ambao hawakuweza kuhudhuria shule kwa sababu ya maswala ya kiafya.

**Masharti ya kuendelea katika kiwango cha shule ya upili cha chini**

Mwanafunzi ataendelea katika mwaka mwingine wa shule iwapo ripoti yake ya tathmini haitoonyesha zaidi ya gredi mbili zisizo ridhisha. Ripoti isionyeshe zaidi ya gredi moja isiyoridhisha katika somo la Kijerumani, Kifaransa au Hisabati. Iwapo mwisho wa mwaka wa shule mfumo huu wa kuenda mbele hatokuwa umeridhishwa basi mwanafunzi atateuliwa tena katika kiwango cha chini cha shule au atahitajika kurejelea hilo darasa katika shule ya aina hiyo. Mwanafunzi hubadilisha shule iwapo kuna sababu ya kuamini kwamba ataweza kukidhi mahitaji hayo.

**Wanafunzi wa Realshule**

Wanafunzi wa aina ya shule ya *Realschul*e wanaweza rejelea mwaka wa 7 katika aina ya shule ya *Sekundarschule* iwapo kuna sababu ya kufikiria kwamba wataweza kukidhi mahitaji.

Wanafunzi wa *Realschule* wanaweza rejelea mwaka wa shule iwapo, hawajapata alama za kupita katika masomo mengi kwenye ripoti ya tathmini.

**Uhamisho kwa shule katika kiwango cha juu cha shule ya upili.**

Kwa wanafunzi ambao wangependa kuhudhuria shule ya baccalaurette au shule ya upili ya juu, uamuazi kuhusu njia za kimasomo hufanywa kati kati ya mwaka wa 8 au wa 9 mtawaliwa. Wazazi hupokea ujumbe zaidi kuhusu mchakato kutoka kwa mwalimu mkuu na walimu kwa wakati ufaao.

**(Seite 9 )**



……………………………………………………………………………………………………………………………………

Kiambatisho 1**: Maana ya alama ni yafwatayo**

| **Alama** | **Kukamilisha kwa malengo yanayohusiana na masomo** | **Kukamilisha kwa mazoezi** | **Kukamilisha kwa kiwango cha ujuzi inayuoambatana na Lehrplan 21** |
|---|---|---|---|
| **6**<br>**Vyema sana** | **Afikia malengo ya masomo kwa vitengo vingi vya ujuzi** | **Mara kwa mara maliza zoezi lenye kiwango cha juu cha ugumu** | **Afikia kiwango cha ujuzi kinachotarajiwa kwa muda1 husika na ujuzi wa zaidi pia katika sehemu za ujuzi wa kibinafsi** |
| **5**<br>**Vyema** | **Afikia malengo ya masomo kwa vitengo vingi vya ujuzi na kwa kiwango flani pia vitengo vigumu kiasi.** | **Mara kadhaa maliza mazoezi yenye kiwango cha juu cha ugumu** | **Afikia kiwango cha ujuzi kinachotarajiwa kwa muda1 husika, kwa sehemu zote za ujuzi.** |
| **4**<br>**Ridhisha** | **Afikia malengo ya masomo kwa vitengo kadhaa vya ujuzi** | **Ipasavyo maliza mazoezi yenye kiwango cha msingi cha ugumu** | **Afikia kiwango cha ujuzi kinachotarajiwa kwa muda1 husika, kwa sehemu nyingi za ujuzi.** |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **3<br>Hairidhishi** | **Feli kuafikia malengo ya masomo kwa vitengo kadhaa vya ujuzi** | **Feli kumaliza mazoezi yenye kiwango cha msingi cha ugumu ipasavyo** | **Kosa kuafikia kiwango cha ujuzi kinachotarajiwa muda[1] husika katika sehemu nyingi za ujuzi.** |
| **2<br>Mbaya** | **Feli kuafikia malengo ya masomo kwa vitengo vingi vya ujuzi** | **Feli kumaliza mazoezi karibia yote yenye kiwango cha msingi.** | **Feli kuafiikia kiwango cha ujuzi kinachotarajiwa kwa muda[1] husika katika sehemu nyingi za ujuzi.** |
| **1<br>Mbaya zaidi** | **Feli kuafikia malengo ya masomo kwa vitengo vyote vya ujuzi** | **Feli kabisa kumaliza mazoezi yote yenye kiwango cha msingi** | **Feli kuafiikia kiwango cha ujuzi kinachotarajiwa kwa muda[1] husika katika sehemu zote za ujuzi.** |

1 Kiwango cha msingi kitatumilka katika mwisho wa mwaka wa 2 na mwaka wa 6 katika kiwango cha msingi na mwisho wa mwaka wa 9 katika kiwango cha chini cha shule ya upili

**(Seite 10 )**

**Tathmini katika kiwango cha msingi na kiwango cha chini cha upili**

**……………………………………………………………………………………………………………………………………………**

## Kiambatisho 2: **Njia ya tathmini katika kila kiwango**

Form view : www.erz.be.ch/beurteilung - Downloads

| **Mwaka wa shule** | | **Mwanzo wa mwaka wa shule** | **Katikati ya mwaka wa shule** | **Mwisho wa mwaka wa shule** | **Uamuzi kwa njia binafsi kwa masomo ambazo zinaweza zipapigwa , zinaweza kuchukuliwa wakati wowotekatika mda wote wa masomo ya lazima** |
|---|---|---|---|---|---|
| **KG 1** | Mviringo wa 1 Shule ya chekechea/Kiwango cha msingi | Mkutano wa walimu na wazazi* | | | |
| **KG 2** | | Mkutano wa walimu na wazazi* | | | |
| **1** | | Mkutano wa walimu na wazazi* | | | |
| **2** | | Mkutano wa walimu na wazazi* | Ripoti ya tathimini Bila alama | | |
| **3** | **Mviringo wa 2 Kiwango cha msingi** | Mkutano wa walimu na wazazi* | | | |
| **4** | | Mkutano wa walimu na wazazi* | Ripoti ya tathmini na alama. | | |
| **5** | | Mkutano wa walimu na wazazi* | Ripoti ya tathmini na alama. | | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **6** | | Mkutano wa kuchaguliwa **<br>Shule ya upili ya chini uamuzi wa kuchaguliwa/-ripoti ya kuchaguliwa<br>Mtihani wa tathmini tena unapohitajika | Ripoti ya tathmini na alama. | | |
| **7** | **Mviringo wa 3 shule ya upili ya chini** | Mkutano wa walimu na wazazi* | Ripoti ya tathmini na alama. | | Kuinginepo ya ujuzi wa kibinafsi na ujuzi muhimu |
| **8** | | Mkutano wa walimu na wazazi* | Uamuzi wa kuchaguliwa : baccalaureate ama schule ya ufundi wa baccalaureate | Ripoti ya tathmini nazo alama | |
| **9** | | Mkutano wa walimu na wazazi* | Uamuzi wa kuchaguliwa : akademia ama shule ya ufundi ya baccalaureate | Ripoti ya tathmini na alama na cheti cha kuhitimu | |

*Shule zina uhuru wa kupanga wakati na tarehe za mikutano ya walimu na wazazi. Wazazi wanaarifiwa kuhusu mikutano iliyopangwa awali ipasavyo.

**Katika kitengo cha msingi, mikutano ya uteuzi ni mwaka wa 6 and hufanyika kabla ya katikati ya Februari.